

TUSIACHE KUSHUHUDIA MBELE ZA
WATU WATENDO MAKUU
ALIYOTUTENDEA BWANA YESU.
MAANDIKO YOH. 9:6-39

1. Mtu mzima yeyote kiroho lazima asione haya **kuyashuhudia** matendo makuu ya Mungu aliyoyatenda katika maisha yake kama anataka kuuona utukufu mkubwa zaidi wa Mungu katika maisha yake

- Kuna wateule wengi ambao leo wanaona kwamba kushuhudia matendo makuu ambayo Mungu ametenda juu yao kama kujitangaza!!

Kuna siri kuu 2 katika kisa hiki baada ya mtu huyu kushuhudia bila aibu matendo makuu aliyomtendea Yesu

a. **Walimtenda katika Sinagogi. Yoh 9:34 (kutengwa na dini zetu za mwanzo)** ni jambo la lazima endapo tutataka kudumu katika kweli ya injili ya Kristo)

- Ukisimama na kweli kabisa ya injili ya Kristo hakuna dini itakayokukubali uendelee kuwa mshirika wake

b. Walipomtenga na Sinagogi (dini) yao Yesu Kristo akamkaribia na kuzungumza nae na akamwona kwa macho yake na akabarikiwa zaidi. **Mst 35-38**

2. Mfalme Daudi katika maisha yake alipenda sana kuyashuhudia matendo makuu ya Mungu aliyoyatenda katika maisha yake. **1Samwl 17:31-37, Zab 9:1 na 118:17.** Mfalme Daudi alifahamu kuwa hai kuwa halisi kwake aendelee kuishi katika dunia hii kutokana na jinsi

alivyowindwa na kuwa katika hatari ya kuuawa wakati wote.
1Samwl 21:10-15, 24:1-15, 26:1-20.

3. Walipenda sana kuyashuhudia matendo makuu. **Mdo 4:17-19, Mdo 26:1-29** n.k “**kwa nini hatuna muda wa kutosha wa kusimulia pamoja na kushuhudia matendo makuu nay a ajabu ambayo Yesu ameyatend katika maisha yetu na badala yake tunasimulia na kushuhudia kazi za adui zaidi katika maisha yetu!!**

- Sote tunafahamu fika kwamba, kama siyo Bwana kuwa upande wetu!! **Zab 124:1-3**

- Leo hii kupata watu wa kusimulia/ kushuhudia matendo makuu ya Mungu katika maisha yao mpaka **ubembeleze!!** Na kama inakuwa hivi mbele ya wateule wenzako, mbele ya Mataifa inakuwaje?? Ina maana Yesu hatendi mambo makuu na ya ajabu katika maisha yetu ambayo kama siyo yeye hata hapa tulipo na hai tuliyonayo iisingewezekana!! **1Samwl 2:1-8**

Na

Askofu Dr. L. M. Mwizarubi

6/4/2022.